

KUTANA NA SARIAH!




Kumfuata Yesu huko Zimbabwe

Jinsi Sariah Anavyomfuata Yesu

Sariah ana matatizo ya kiafya. Anatumia dawa kumsaidia. Ana shukrani kwa ajili ya maisha yake. "Mwokozi ananisaidia, kwa hiyo hakuna haja ya kuwa na wasiwasi," anasema.

"Wakati mama yangu anapokuwa amechoka, huwa anahitaji mtu wa kucheza na dada yangu mdogo," anasema Sariah. Anasaidia kwa kumwimbia, kumbeba na kucheza naye.

Sariah ni wa kwanza kutambua wakati mama yake ana huzuni, na daima humkumbatia kwa nguvu. "Kuwasaidia watu kunanifanya niwe na furaha," anasema. "Hususan kuisaidia familia yangu." ●



Wewe Pia Unaweza Kumfuata Yesu!



Ni kitu gani umefanya ili kumfuata Yesu? Andika na utueleze! Geuza jalada la nyuma ili kuona jinsi ya kufanya hilo.



Mhoroi!



Kuhusu Sariah

UMRI MIAKA: 7

KUTOKA Mashariki mwa Mashonaland, Zimbabwe

LUGHA: Kiingereza, Kishona,

MALENGO: 1) kuwa mcheza dansi. 2) Kuwa daktari.

JAMBO ALIPENDALO: kucheza na marafiki

FAMILIA: Sariah, Mama, Baba, kaka mkubwa, dada mkubwa, dada mdogo

Mambo Ayapendayo Sariah

HADITHI YA KITABU CHA MORMONI: Wakati Yesu Kristo alipowabariki watoto wa Kinefi (ona 3 Nefi 17.)

SIKUKUU: Pasaka

MATUNDA: Matufaa na zabibu

RANGI: Nyekundu

WIMBO WA WATOTO: "The Sixth Article of Faith" (Kitabu cha nyimbo za watoto, 126).